KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 10, Issue 3

17th Jumâ dal-Aakhir 1432

20th May, 2011

YALIYOMO

Makosa Arubaini Yanayohusiana Na Swala 1 - 3

MAKOSA ARUBAINI YANAYOHUSIANA NA SWALA [Prt 2]

Sheikh Saalih Ibn Abdul-Azeez Ibn Muhammad Aali-Shaykh

19 KUJISHUGHULISHA NA MAMBO YENYE KUKUTOA KWENYE SWALA

Huu ni ushahidi wa mtu kupenda mambo ya ulimwengu kuliko Akhera, kuandama mambo ya upotofu na kujishughulisha na kutomtwi'i Allaah (سبحانه وتعالى): **"Enyi mlioamini yasikusahaulisheni mali yenu wala watoto wenu kumkumbuka Allaah na wafanyao hayo, hao ndio wenye kukhasirika."** [al-Munafiqoon-63:9].

Na akasema katika kuwasifu waumini: **"Watu ambao biashara wala kuuza hakuwashughulishi (hakuwasahaulishi) kumkumbuka Allaah, na kusimamisha swala, na kutoa zaka."** [an-Noor-24:37]. Kufanya lolote lenye kusababisha kuharibu swala au kumfanya mtu asijali au kufanya uvivu katika kuitekeleza kama kukaa usiku mkubwa na mfano wake, hilo haliruhusiwi. Hii ni kwa sababu chochote chenye kumpeleka mtu katika haraam basi nacho ni haraam. Na Allaah ndie aongozae katika njia ya sawa.

20 KUCHEZEA NGUO AU SAA NA VITU KAMA HIVYO.

Hiki ni kitendo kiondoshacho khushoo' na dalili ya khushoo' imeshatangulia kutajwa katika no.5- Mtume (صلى الله عليه وسلم) amekataza kupangusa changarawe wakati wa swala kwa sababu yaondosha athari ya khushoo' aliposema: "Yoyote miongoni mwenu anayeswali na asifute changarawe kwani Rehma humteremkia yeye" [Ahmad na mikusanyo sita ya hadeeth kwa sanad iliyo swaheeh]. Mtu huenda akazidisha kucheza-cheza mpaka harakati zake zikapita kiyasi nje ya swala na akaharibu swala yake.

21 KUFUNGA MACHO BILA YA SABABU.

Hiki ni kitendo cha kuchukiza (makrooh) kama alivyotaja Ibn al-Qayyim: "Kufunga macho si katika muongozo wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Pia alisema: "Wanazuoni wa fiqh wamekhitilafiana juu ya utukivu wake. Imaam Ahmad (رحمه الله) na wengine waliona kuwa ni kitu cha kuchukiza na wakasema kuwa ni katika tabia za Mayahudi. Ingawaje, wengine waliruhusu bila ya uchukivu na wakasema huenda ikawa ni katika njia za kuipata khushoo', ambayo ndicho kiini, moyo na malengo ya swala'. Lililo la sawa zaidi ni kwamba ikiwa kufungua macho hakutoleta madhara yoyote katika kuipata khushoo', basi yapendekezwa kufanya hivyo. Ikiwa marembo na manakshi na mifano yake iko mbele baina yake na kibla basi hapana ubaya hata kidogo kuyafumba. Na kwa hakika rai ya mustahab (kupendeza) katika hali ya kuyafumba ni karibu na mwito wa sheria na malengo yake kuliko rai yakuwa haifai. Na Allaah ni Mjuzi zaidi.

22 KULA, KUNYWA NA KUCHEKA KATIKA SWALA HUIVUNJA SWALA.

Ama kuhusu kula na kunywa kuna maafikiano kuhusu fardh. Ibn al-Mundhir amesema: "Wanavyuoni (Ahlul-'Ilm) wameafikiana yakwamba mwenye kuswali haruhusiwi kula na kunywa. Na vile-vile wameafikiana miongoni mwao yakwamba kufanya

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

hivyo kwa kukusudia inawajibisha kurudiwa kwa swala." Ibn al-Mundhir pia akapokea kuwa kuna ijmaa' (maafikiano) yakwamba swala yaharibika kwa kucheka.

23 KUPAAZA SAUTI KATIKA KUSOMA MPAKA UKAWATATIZA WALIOKO KANDO YAKO

Imependekezwa (mustahabb) yakwamba mtu ajisikie mwenyewe, kiasi cha kutowashawishi wenzako wanaosoma Qur'an au walio katika swala. Al-Bukhaari na Muslim, wote wamepokea kutoka kwa Umraan Ibn Husain (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliswali adhuhuri na palikuwa na mtu nyuma yake akisoma 'sabbihisma rabbikal-a'laa' basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipomaliza kuswali akauliza: "Ni nani miongoni mwenu aliyekuwa akisoma au ni nani msomaji?" yule mtu akasema: "Ni mimi." Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Nilidhani yakwamba baadhi yenu mwashindana na mimi." Wanavyuoni wamesema: "Maana ya maneno yake ni kukataza kufanya hivyo. Ibn Taymiyah (رحمه الله) amesema: "Yoyote anayesoma Qur'an na watu wakawa wanaswali swala za ziyada, basi ni makosa kusoma kwa sauti kubwa hivyo kuwasumbua wenzake kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwaacha baadhi ya Maswahaba wake walipokuwa wakiswali as-Sahr (kabla ya alfajiri) na akasema: "Enyi watu, kila mmoja wenu ataka kutoka kwa Mola wake uongofu, basi musitenzane nguvu katika kusoma kwenu."

24 KUWAKUSANYIKIA WATU WANAOSWALI

Hiki ni kitendo kikatazwacho katika kuwadhuru watu. Ni juu ya mwenye kuswali aswali palipo na nafasi ila akiona pana nafasi iliyowachwa aweza kuifuatia ikiwa iko njia. Ama kuleta dhiki haswa siku ya ijumaa kwa ujumla haifai. Alisema Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwahusu wale wenye kuzikata swafu za swala: "Keti chini hakika umedhuru na umechelewa."

25 KUTOZINYOSHA SWAFU KISAWASAWA

Allaah ameamuru kuziimarisha swala kisawasawa, akasema: "Na simamisheni (aqeemu) swala." Vile-vile Mtume (صلى الله عليه وسلم) amehimiza kunyoosha swafu akasema: "Nyosheni swafu zenu, kwani kwa hakika unyoshaji wa swafu ni katika sehemu ya usawa wa swala (iqaamis-salaah)" - kutoka kwa Anas (رضي الله عنه) [al -Bukhaari na Muslim]. Vile-vile al-Bukhari amepokea kutoka kwa an-Nu'maan Ibn Basheer (رضي الله عنه): "Nyosheni swafu zenu au Allaah atazifanya nyoyo zenu kuhitilafiana." Amri ya kunyosha swafu na kuwa na hadhari katika kutkeleza hilo imetajwa kwenye idadi kadhaa ya hadeeth (na pia ijulikane yakwamba jambo hilo linahusu kutowacha pengo yoyote baina ya swafu kama jinsi inavyopuuzwa mara nyingi).

26 KUINUA MIGUU KUTOKA KWENYE ARDHI WAKATI WA SUJOOD.

Huku ni kwenda kinyume na maamrisho kama ilivyo katika swaheeh mbili kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliamrishwa kusujudu juu ya viungo saba na kutozifunga nywele zake wala kukunja nguo anapokuwa kwenye swala. Bapa la uso (ikiwemo pua), vitanga viwili vya mikono, magoti na miguu miwili. Kwahivyo mwenye kuswali ameamrishwa kuswali kwa miguu miwili ikigusa ardhi na njia ya ukamilifu wa kutekeleza hivyo ni kuvifanya vidole vya miguu vielekee Qiblah. Sehemu ya kila mguu na iguse ardhi na lau mtu atauinua mmojawapo, basi sijdah yake itakuwa ni ya makosa iwapo ataendelea kufanya hivyo katika sijdah yote.

27 KUWEKA MKONO WA KULIA JUU YA MKONO WA KUSHOTO NA KUIINUA MPAKA SHINGONI

Huku ni kuikhalifu Sunnah kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wake wa kushoto juu ya kifuaa chake. Hii iko katika hadeeth ya Hasan kutoka kwenye mapokezi mengi yaliyo dha'eef lakini kwa ujumla zatiliana nguvu. Sunnah vilevile ni kuweka mikono kati-kati ya kifua au juu ya moyo kwa sababu moyo uko kifuani kama asemavyo Allaah (سبحا نه وتعالى): "Ni nyoyo zilizo ndani ya vifua, zenye upofu." Kuinua mikono (kupiga takbeer) wakati wa kwenda kwenye sujood au kuinuka kutoka kwenye sujood. Ni makosa kuinua mikono mpaka shingoni na hili lapinga Sunnah. Kilicho nasibiishwa kwa 'Ali (رضي الله عنه) katika kuileza aya isemayo: "Kwa hivyo swali kwa Mola wako na uchinje (wanhar - ambapo tendo likapindwa mpaka likamaanisha shingo [an-nahr]) ni dhaifu na wala haina misingi ya ushahidi (pia vitendo vya kuweka mikono chini ya kitovu na kushika visukusuku hakuna ushahidi wa hayo katika Sunnah).

28 KUINUA MIKONO WAKATI WA KWENDA SUJOOD AU KUTOKA.

Huku ni kwenda kinyume na Sunnah iliyo maarufu iliyopokewa na wengi wa Maswahaba waliopokea kuhusu kuinua mikono. Wanafunzi wa 'Ilmu ya Sharee'ah na wajilazimishe juu ya Sunnah zilizo maarufu isipokuwa kwa siri ingawa aamini kuwa kitendo hicho ni sawa zaidi kutokamana na Sunnah ambayo isiyokhalifu vitendo kwa ujumla wa wanavyuoni. Imaam wa watu afanye kinachojulikana (katika Sunnah swaheeh), kwani kilicho maarufu na kujulikana sana kuwa ni Sunnah yenye kufanywa na wengi wa wanavyuoni, ni yenye kutosheleza na

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

kuridhisha. (hikma hapa ni kwamba kwa mwanafunzi kusisitiza kufanya mambo hadharani ambayo wanavyuoni kwa ujumla hawaoni kuwa ni Sunnah huwenda ikaleta utata na kusababisha michafuko, jambo ambalo linaweza kusababisha kuwachana na faradhi, Yaani kuzuia madhara kwa ajili ya kuisimamisha Sunnah- na ambayo haikubaliwi kabisa katika hiyo - na itaangukia katika makosa. Wanavyooni hawaafikiani juu ya jambo lolote bila ya ushahidi, ingawa mwanafunzi wa elimu mwenye ujuzi anaweza kutokubaliana na amri au maamuzi kulingana na kuelewa kwake juu ya maadishi na baada ya utafiti wa kina na kufikia mahali pa kumtosheleza yeye mwenyewe na matokeo yake.

29 KUHARAKISHA SWALA KWA BAADHI YA MAIMAMU NA UKOSEFU WA UTULIVU NDANI YAKE

Haraka walizo nazo baadhi ya ma-Imaam kwenye swala na ukosefu wa utulivu ndani yake, hivyo-basi, wasiwape fursa ma'mooma kuwa na utulivu katika swala zao au wakati wa kuisoma al-Faatiha, hususan katika rakaa'a ya mwisho. Imaam ana jukumu la kuifanya swala ya wenye kumfuata iwe nzuri kwa sababu yeye hufuatwa. Kwahivyo ni jukumu lake kuwa muangalifu katika kuitekeleza Sunnah, na kuwa na utulivu ndani yake ni nguzo (rukn) ambayo Imaam anawajibika zaidi kuwa na tahadhari kutokana na kufuatwa kwake. Vile vile usomaji wa al-Faatiha ni rukn ambayo maamuma ni lazima wapewe fursa ya kutosha kuitekeleza. Tumeshatangulia kueleza dalili za uwajibikaji wa kuwa na utulivu (*tuma'neenah*) *na kuisoma Surat al-Faatiha*

30 KUTOKUWA MUANGALIFU KATIKA KUSUJUDU KWA VIUNGO SABA.

Viungo vyenyewe saba ni bapa la uso, pamoja na pua, vitanga viwili vya mikono, magoti mawili na vidole vyote vya miguu miwili. 'Abbaas Ibn Abdul-Muttwalib (رضي الله عنه) alihadithia yakwamba alimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: "Anaposujudu mja, husujudu nae viungo saba; Uso wake, mikono, magoti yake mawili, na miguu yake miwili. [Muslim] (pia imenasibishwa na Al-Majd katika "Al-Muntaqaa" Al-Muzee na imepokewa na wengine. Ibn 'Abbaas amepokea: Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Nimeamrishwa kusujudu juu ya 'mifupa' saba (yaani; sehemu za mwili) kwa bapa la uso - na akaashiria kwenye pua yake - mikono miwili, magoti mawili, na miguu miwili. Kuna baadhi wa watu wasiosujudu kwa bapa la uso wala kwa pua, au wenye kuinua miguu yao au ambao viganja vyao vya mikono visivyogusa ardhi, yote hayo yakiwa ni kinyume cha yaliyoamrishwa.

31 KUTOJALI KUJIFUNZA HUKMU NA SHERIYA ZA SWALA

Hili ni jambo ambalo Muislamu yoyote haifai kufanya hivyo. Bila shaka swala ni nguzo iliyo kubwa katika nguzo za Uislamu inayohitaji vitendo vya mwili. Allaah ameamrisha kusimamishwa - "Aqimis-Salaah" (simamisheni swala) katika zaidi ya aya sabiini. Haiwezekani kuitekelezwa bila ya kuwa na 'ilmu ya misingi yake au kutojuwa vipi Mtume (صلى الله عليه وسلم) alivyoitekeleza. Hakuna nafasi ya ujinga kuhusu hukmu za swala, kujua yanayopasa au yalioyo wajibu juu yake, hukmu za kufuata au kurekebisha makosa yatokeyao na mfano wake. Ni faradhi kuyajua mambo hayo na ukosefu wa 'ilmu ya mambo haya ndio sababu ya Muislamu kutoyajuwa yanayobatilisha na kuharibu swala yake. Na twamuomba Allaah Uongofu na Mafanikio.

32-34 KUTOJALI KATIKAUSOMAJI NDANI YA SWALA

Kuzembea katika kusoma al-Faatiha tena kwa usomaji wa kisawasawa kama vile kusoma *al-'Aalimeen* badala ya *al-'Aalameen, ahdinaa* badala ya *ihdinaa*, *an'amtu* badala ya *an'amta*, na kuendelea. Haya yote na makosa mfano wake ni katika sampuli za makosa ya kilugha ambayo ni lazima yaepukwe na yoyote mwenye kuswalisha. Na matamshi mengine yana maana yasiowezekana kama vile mtu anapotamka "t" (taa') katika "an'amta" kama "da" (daad) na kwahivyo swala ikawa imeharibika.

35 KUALISHA VIDOLE NDANI YA SWALA.

Hili ni katika mambo yachukizayo kwenye swala na kwahivyo limekatazwa. Ama kuhusu kuvialisha kwa ujumla, Ibn Abee Shaybah akapokea kwenye maneno kwa sanad swaheeh, kutoka kwa Shu'bah Mawlaa Ibn Ibn 'Abbaas akisema: "Niliswali karibu na Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) na nikaalisha vidole vyangu, basi nilipomaliza swala akasema. "Mwana kukoswa na mamako! Wavunja vidole vyako ukiwa kwenye swala?" Makatazo ya kualisha vidole katika swala yamepokewa kwa hadeeth marfoo' kutoka kwa 'Ali katika sunnan ya Ibn Majah, lakini ni dhaifu na haijitoshelezi yenyewe (ghairu munjabir).

36 KUVIKUMBATISHA VIDOLE (AT-TASHBEEK) UNAPOKUWA KWENYE SWALA NA BAADA YAKE

Haya pia ni katika mambo yenye kuchukiza. Ka'ab Ibn 'Ujrah (رضي الله عنه) amehadithia: "Nilimsikia Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: 'Anapotawadha mmoja wenu kisha akenda msikitini kwa ajili ya kuswali, na asiikumbatishe mikono yake pamoja kwani kwa hakika yeye huwa yuko ndani ya swala. [Ahmad, Abu Daawud, At-Tirmidhi]. Ikiwa na tafauti

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 4)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

katika silsila yake, Ad-Daarimi, Al-Haakim na wengineo wamepokea kutoka kwa Abu-Hurayrah kwa hadeeth iliyo Marfoo': "Anapotawadha mmoja wenu akiwa nyumbani kwake kisha akaja msikitini, huwa yuko ndani ya swala mpaka atakaporudi. Kwahivyo musifanye hivi - na akavikumbatisha vidole vyake pamoja." Kuna hadeeth nyengine zenye kusaidiana katika mas'ala haya ya tashbeek.

37 KUMSUKUMA MTU MBELE ILI AONGOZE SWALA WAKATI SI MAHALI PAKE NA KUNA WENGINE WANAOSTAHIKI.

Kumuweka mtu mbele aongoze swala kama Imaam haliyakuwa hastahiki kuwa hapo na ikawa kuna wenye kustahiki kuliko yeye. Huku ni kwenda kinyume na malengo ya kuwa na Imaam (al-Imaamah), ambako ni kuwa kielelezo cha kuandamwa (al-iqditaa'). Ni jambo la lazima yakwamba Imaam awe na ufahamu wa dini na awe na uwezo wa kuisoma Qur'an sawasawa kulingana na maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Imaam wa watu anafaa awe mbora wao katika kuisoma Qur'an.." Imepokewa na Muslim kutoka kwa Abu Mas'ood Al-Answaari (رضي الله عنه). Wanavyuoni wamehukumu yakwamba hafai kumfanya mtu kuwa ni Imaam ambaye kusoma kwake ni kwa makosa, au anayeonyesha wazi ma'asiya au mwenye tabia za ukosefu wa adabu, au ambaye ni mzushi, au ambaye ni mwenye kuleta uharibifu kama wao. Ingawaje, lau kama watu kama mfano wake watawekwa mbele, swala ya ma'mooma itakuwa iko sawa.

38 KUTOISOMA QUR'AN VIZURI

Hii ni kasoro iliyo wazi na haki za Qur'an ni kwamba na isomwe kisawasawa pasi na makosa na kwamba Waislamu wanafaa kujitahidi na kutekeleza usomaji kwa njia ipasayo. Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: "Isome Qur'an kwa tarteel." Na: "Tunapokusomesha Qur'an, fuatiliza usomaji wake." Ikimaanisha usomaji kama ilivyo sawa kulingana na lugha ya kiarabu, kwa uwazi bila ya kupotoa. Katika mstari huu huu ni utukufu wa yule anayesafisha niya yake kama ilivyopokewa na 'Aaisha (رضي الله عنها) aliyesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Mwenye ujuzi wa kuisoma Qur'an vizuri atakuwa na waandishi (Malaika) walio watukufu na watwi'ifu. Na mwenye kuisoma Qur'an kwa kusitasita na kupata tabu (katika kujaribu kuisoma kisawasawa) atapata thawabu mara mbili." [Muntafaqun 'alayh]

39 BAADHI YA WANAUME KUSWALI NYUMA YA WANAWAKE KATIKA HARAM (MAKKAH)

Kufanya hivyo hapo na penginepo ni kitendo chenye kuchukiza katika swala. Ni katika Sunnah kuwa swafu za wanaume ziwe mbele za swafu za wanawake. Swala ya mwanamume nyuma ya mwanamke huwenda ikamsababisha kukosa khushoo' yote na ni usumbufu wa moyo katika swala kwa kule kumtizama mwanamke au vyenginevyo. Kwahivyo mwanamume hafai kujipanga kwa swala akiwa nyuma ya mwanamke. Hili likiwa ni dharura basi yakubalika kama kuchelea kuikosa swala ya 'Eid au ljumaa au ya Jamaah na mifano mengine yenye kufanana na hayo. (ambao yaleta kutowezekana kuunga safu za mbele za waume- pamoja na hivyo isiwe karibu). Baadhi ya wanavioni wamesema 'Haraam ya Makkah ni hali nyingine na yakubalika." Shaykh Abdul-Azeez Ibn Baaz (رحمه الله) yuko kwenye rai hii.

40 WANAWAKE KUJA MISIKITINI WAKIWA WAMEJIPAMBA

Mambo haya ni miongoni mwa maovu yalio wazi na yenye kudhihirika wakati wa Ramadhani na nje yake. Wanawake huja misikitini kumuabudu Mola wao, na wala sio kujionyesha marembo ya maguo yao! Huwenda waume wakamuona akapata madhambi na akakosa malipo ya kitendo chake. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Mwanamke yeyote atakaejitia manukato, na asije kuungana nasi katika swala ya 'Ishaa." [Muslim] na Imaam Ahmad na Abu Daawud wamepokea kwa sanad swaheeh kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Msiwakataze wanawake huru wa Allaah kuja katika nyumba ya Allaah na waacheni wende nje tafilaat." Maana ya kilma "tafilaat" ni wasiwe wamejirembesha na marembo na manukato.

NENO LA BUSARA

Amesema Allaah (سبحانه وتعالى)

"Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu; basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Allaah, (msipuuze jambo la kupatanisha) ili mrehemewe."

[Surat al-Hujuraat, (49): 10]